# Mwongozo wa Marejeleo ya Haraka ya Kutoa Bili ya Mtoaji wa Huduma

Bili ya mtoaji wa huduma huwasilishwa baada ya utunzaji kukamilika, lakini siyo mapema kabla ya Ijumaa 5:00 jioni kwa mujibu ya ratiba ya kila wiki ya kutoa bili. Ili bili ichakatwe wiki hiyo ni lazima iwasilishwe kufikia Jumatano Adhuhuri. Ili bili ilipwe ni lazima iwasilishwe ndani ya siku 60 za wakati wa mwisho wa kuwasilishwa uliowekwa. Pindi ikiwasilishwa bila makosa, Idara itamlipa mtoaji wa huduma za kutunza watoto ndani ya siku ishirini baada ya kupokewa. Maelezo yaliyo hapa chini ni mwongozo wa marejeleo ya haraka ya kutoa bili. Kwa maelezo kamili rejelea Makubaliano ya Mtoaji wa Huduma na Kanuni za Ruzuku ya Utunzaji wa Watoto.

## Ufafanuzi wa Safu

**Ada ya Mzazi ya Sasa N/H** – Sehemu ya mzazi iliyolipwa kwa mtoaji wa huduma na mzazi. *Katika wakati huu ada zote za wazazi zinagharamiwa na Sheria ya Kuimarika na Kuwekeza Upya ya Marekani (ARPA). Tafadhali ingiza N.*

**Saa za Kawaida –** Jumla ya saa ambazo mtoto alihudhuria ana kwa ana kwa wiki kati ya 6:00 asubuhi - 6:00 jioni. Jumatatu-Ijumaa.

**Saa Zilizo na Udhuru–** Kutohudhuria ambako unajua kuhusu na ni lazima kuandikwe kwenye fomu. **Sababu Inayokubalika** inamaanisha sababu Zilizoidhinishwa na Idara za Mtoto kutohudhuria programu ya Mtoaji wa Huduma za Kutunza Watoto ambazo zinaweza kujumuisha, bila kikomo kwa: Sikukuu za Shirikisho/Jimbo; siku za likizo ya wazazi; hali ya hewa ya baridi kali inayobainishwa na siku yenye theluji ambayo shule za eneo husika zimefungwa; Mtoto kuwa mgonjwa au Mwanafamilia wa karibu; miadi; matatizo ya usafiri ambayo yanaathiri uwezo wa Mzazi wa kumsafirisha mtoto hadi kwa kituo cha Utunzaji, ziara za Familia: Dharura za Familia, ikiwemo lakini bila kikomo kwa, upasuaji, matibabu, au ajali; au matukio ya misiba yanayoathiri Familia, ikiwemo lakini bila kikomo kwa, moto, dhoruba, au ajali

*Kupitia kwa ARPA, CCSP alianza kutoa bili kwa ajili ya uandikishaji dhidi ya uhudhuriaji. Saa za Kawaida zitakuwa saa halisi ambazo mtoto amehudhuria na Saa Zilizo na Udhuru zitakuwa saa zilizoongezwa ili kumfikisha mtoto kwa uidhinishaji wa juu zaidi unaoruhusiwa kama ilivyoidhinishwa katika barua ya ruzuku ya masomo.*

*Mfano: Jane Doe ni mtoto aliye na umri wa kwenda shuleni na amepewa ruzuku ya hadi saa za wakati kamili (saa 30). Kwa kawaida Jane uhudhuria huduma za kutunza watoto kwa wakati kamili katika majira ya joto na kwa sehemu ya wakati katika mwaka wa shule, Jumatatu 7-8 asubuhi, Jumanne 8 asubuhi-5 jioni, Jumatano 7-8 asubuhi, Alhamisi 8 asubuhi-5 jioni, Ijumaa 7-8 asubuhi kwa jumla ya saa 21 kwa wiki. Fomu ya kutoa bili wakati wa mwaka wa shule itasema Saa 21 za Kawaida na Saa 9 Zilizo na Udhuru ambazo zitakuwa na jumla ya saa 30 za wakati kamili.*

**Siku Zilizo na Udhuru -** ruka

**Saa Zisizo na Udhuru -** Kutohudhuria Kusikoruhusiwa kunamaanisha Mtoto kutohudhuria kwenye Huduma ya Kutunza Watoto kwa zaidi ya siku mbili (2) za kalenda kwa mwezi bila Sababu Inayokubalika au uidhinishaji wa awali kutoka kwa Idara.

**Likizo ya Mtoaji wa Huduma** Ili kudumisha uendelevu wa Huduma za Kutunza Watoto, katika kipindi cha miezi kumi na miwili (12) (Januari hadi Januari), Idara itamlipa Mtoaji wa Huduma za Kutunza Watoto kwa: sikukuu za jimbo na hadi saa hamsini (50) za wakati wa likizo ya Mtoaji wa Huduma za Kutunza Watoto kama inavyohitajika kwa sheria ya shirikisho (45 C.F.R. §98.45)

**Mafunzo ya Mtoaji wa Huduma** Ili kudumisha uendelevu wa Huduma za Kutunza Watoto, katika kipindi cha miezi kumi na miwili (12) (Januari hadi Januari), Idara itamlipa Mtoaji wa Huduma za Kutunza Watoto kwa: hadi saa arobaini (40) za mafunzo.

**Siku Zisizo na Udhuru –** ruka

**Saa Zisizo za Kazi –** Utunzaji unaofanyika baina ya 6:00 jioni hadi 6:00 asubuhi na wikendi. Malipo ya ziada ya 35% ya kiwango cha msingi cha watoaji wa huduma kwa saa zilizotumiwa yatalipwa)

**Jumla ya Saa- idadi ya jumla ya saa za utunzaji kwa wiki – Jumlisha**

**Kutohudhuria Kusikoruhusiwa** kunamaanisha kutohudhuria kwa Mtoto katika Huduma ya Kutunza Watoto kwa zaidi ya siku mbili (2) za kalenda kwa mwezi bila Sababu Inayokubalika au uidhinishaji wa awali kutoka kwa Idara

**Kipindi cha Kutoa Bili cha Wiki 2: 9/25/2021 – 10/1/2021**

| Mtoto | Kikundi cha Umri | Ada ya Sasa ya Mzazi N/H | Saa za Kawaida | Saa Zilizo na Udhuru | Siku Zilizo na Udhuru | Saa Zisizo na Udhuru | Likizo ya Mtoaji wa Huduma | Mafunzo ya Mtoaji wa Huduma | Siku Zisizo na Udhuru | Saa Zisizo za Kazi | Jumla ya Saa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mtoto anayeanza kwenda dede | | | | | | | | | | |
| | Mtoto mchanga | | | | | | | | | | |
| | Mtoto ambaye hajaanza kwenda shuleni | | | | | | | | | | |

Mtoto mchanga inamaanisha mtoto aliye na umri wa wiki 6 hadi miezi kumi na miwili (12)
Mtoto anayeanza kwenda dede ni mtoto aliye na umri wa miezi kumi na mitatu (13) hadi miezi thelathini na sita (36)
Mtoto ambaye hajaanza kwenda shuleni ni mtoto ambaye ana umri wa zaidi ya miezi 36 lakini hajaandikishwa katika Shule ya Chekechea bado
Mtoto mwenye umri wa kwenda shuleni ni mtoto aliyeandikishwa katika Shule ya Chekechea

| | Wakati Kamili | Sehemu ya Wakati | Nusu ya Wakati | Robo ya Wakati |
|---|---|---|---|---|
| Mtoto mchanga/Mtoto anayeanza kwenda dede/Chekechea | Saa 30+ kwa wiki | Saa 20-29 kwa wiki | Saa 10-19 kwa wiki | Saa 0-9 kwa wiki |
| Umri wa Kwenda Shuleni | Saa 30+ kwa wiki | Saa 11-29 kwa wiki | Saa 6-10 kwa wiki | Saa 0-5 kwa wiki |